Nambari ya Mtahiniwa:.....

THE JOINT EXAMINATION FOR CATHOLIC SCHOOLS (JECAS)
FORM II PRE-NATIONAL EXAMINATION September 2019

021 **KISWAHILI**

TIME: 2.30HRS **Monday 16th September 2019a.m**

MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali **kumi (10)**
2. Jibu maswali **YOTE**
3. Majibu yote yaandikwe kwenye nafasi ulizopewa
4. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya wino wa blue au mweusi
5. Vifaa vyote vya mawasiliano HAVIRUHUSIWI katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia

KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU		
NAMBA YA SWALI	**ALAMA**	**SAINI YA MTAHINI**
1		
2		
3		
4		
5		
6		
7		
8		
9		
10		
JUMLA		

Karatasi hii ina kurasa 9 zenye maandishi

Scanned by CamScanner

Nambari ya Mtahiniwa:.....

SEHEMU A (ALAMA 15)
UFAHAMU

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata.

Makazi ni makao au maskani wanamoishi viumbe hai na ni utaratibu mzima wa kila siku wa maisha yao katika eneo hilo. Neno Bora kwa lugha ya kawaida ama humaanisha kufaa, uzuri au thamani ya kitu. Kwa maana hiyo MAKAZI BORA ni maskani yanayofaa au yaliyo mazuri kwa maisha ya viumbe hai.

Ama **mada** yetu inatutaka kuangalia MAKAZI BORA YA WANADAMU. Kwa **muktadha** huo itakuwa ni utaratibu au mwenendo ulio mzuri wa maisha ya wanadamu katika hasua zao. Suala zima la makazi bora linatakiwa lifungamanishwe na maisha mazuri na yenye **hadhi** inayowiana na thamani ya mwanadamu kiutu...

Makazi bora au maisha mazuri havipatikani ila kwa kukamilika mazingira mazuri ya Kijiografia, Kibayolojia, Kisaikolojia na Kiutamaduni. Kijiografia yapaswa kuzingatiwa uoto wa asili na masuala yote ya usambazaji wa miundo mbinu kama vile barabara, umeme, maji, mawasiliano, mfumo wa majitaka na taka ngumu, masoko, machinjio na huduma nyingine muhimu kama shule, zahanati, na vituo vya mabasi.

Kibayolojia mwili ni lazima ufanye kazi na hilo haliwezekani bila chakula tena kilicho bora na cha kutosha, makazi yaliyo mazuri kuanzia ubora wa nyumba hadi makazi. Ubora wa nyumba ni pamoja na jiko la kutosha, vyoo *vizuri na mandhari ya* mbele na nyuma yanayopendeza, yenye kuleta hewa safi.

Mwanadamu ni haki yake kuchoka na vile vile kupumzika, hivyo anahitaji michezo na burudani kuweza kuyabadili angalau kwa muda mazingira yaliyomfanya achoke. Anahitaji majirani ikiwa ni pamoja na kuwa huru kushiriki masuala ya kisiasa na kijamii bila kubaguliwa au kubagua.

Kiutamaduni, mwanadamu sharti azalishe mahitaji yake ya lazima na ashirikiane na wenziwe katika kuyaendeleza makazi yao ili yawe makazi bora na siyo bora makazi. Hii inamlazimu kushiriki kikamilifu katika suala zima la uzalishaji mali ama wa kuajiriwa au kujiajiri.

Hivyo, makazi bora ni yenye kuhakikisha kuwa wakazi wake wanapata fursa ya kujipatia riziki kuongeza mapato kwa maendeleo yao, ya vizazi vyao na taifa kwa ujumla.

Scanned by CamScanner

Nambari ya Mtahiniwa:.....

Ni kwa **mantiki** hil makazi bora hayana budi kutenga maeneo ya viwanda, kilimo, ufugaji, biashara na uchimbaji madini.

MASWALI:

a) Andika kichwa cha habari kinachofaa kwa habari uliyoisoma kisichozidi maneno matano.

_____

b) Orodhesha maneno matatu (3) yaliyotumika katika habari hii yenye maana ya eneo la kuishi

i. _____

ii. _____

iii. _____

c) Eleza kwa ufupi maana ya bora makazi

_____

_____

d) Eleza maana ya maneno yaliyopigiwa mstari kama yalivyotumika katika kifungu cha habari ulichosoma

i. Muktadha _____

ii. Mada _____

iii. Hadhi _____

iv. Mantiki _____

2. *Fupisha habari uliyoisoma kwa maneno yasiyopungua hamsini na yasiyozidi (60)*

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

Scanned by CamScanner

Nambari ya Mtahiniwa:.....

SEHEMU B (ALAMA 20)
SARUFI

3. Eleza dhima mbili kwa kila mofimu iliyopigiwa mstari

a) Aliyefika hapa

_____

_____

b) Mtoto ametoroka

_____

_____

_____

c) Ninakupenda

_____

_____

_____

d) Hataki masikhara

_____

_____

_____

e) Alimtukana

_____

_____

4. Bainisha mzizi wa asili kwa kila neno katika maneno yafuatayo.

a) Shambulia _____

b) Anakula _____

c) Malezi _____

d) Wanakimbizwa _____

e) Mabadiliko _____

f) Ufumbuzi _____

g) Sababisha _____

h) Laza _____

i) Zamisha _____

j) Sanduku _____

Scanned by CamScanner

Nambari ya Mtahiniwa:.....

SEHEMU C (ALAMA 20)
MAWASILIANO NA UTUMIZI WA LUGHA

5. Taja faida tano (5) za lugha ya kimazungumzo

i. _____

_____

ii. _____

_____

iii. _____

_____

iv. _____

_____

v. _____

_____

6. (a) Eleza maana ya utata wa tungo

_____

_____

_____

_____

_____

(b) Taja mambo manne (4) yanayosababisha utata wa tungo.

i. _____

_____

_____

ii. _____

_____

_____

iii. _____

_____

_____

iv. _____

_____

_____

Scanned by CamScanner

Nambari ya Mtahiniwa:.....

SEHEMU D (ALAMA 30)
FASIHI

7. (a) Kamilisha methali zifuatazo
   i. _____ kuliko mali.
   ii. Awali ni awali _____
   iii. _____ si jema la mwenzako.
   iv. _____ haigombi.
   v. _____ halilali nguruwe.

   (b) Eleza maana ya nahau hizi:
   i. Zunguka mbuyu _____
   ii. Mezea mate _____
   iii. Kujikaza kisabuni _____
   iv. Lamba udongo _____
   v. Fua dafu _____

8. Fafanua vipengele vifuatavyo.
   a) Mizungu _____
   _____
   _____
   _____
   _____
   _____

   b) Hadhira _____
   _____
   _____
   _____

   c) Ujumbe _____
   _____
   _____

   d) Miviga _____
   _____

Scanned by CamScanner

e) Ushairi _____

9. Soma utungo ufuatao kisha jibu maswali yanayofuata.

I. Utu na ubinadamu, ni kama yai na kuku,
Utu ni ile nidhamu, Mola aliyokhuluku,
Ubinadamu ni damu, ya utu wa kila siku,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake.

II. Yeyote mwanadamu, ana asili ya utu,
Yani kwenye yake damu, hakikosi hiki kitu,
Utu sifa maalumu, ya mtu kuitwa mtu,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake.

III. Utu wa kweli kwa mja, ni wenzake kuwajali,
Utu huiona haja, ya kujua watu hali,
Utu ni kuwa pamoja, kwenye shida mbalimbali,
Utu wowote wa mtu ni kuwajali wenzake.

MASWALI:

a) Taja wazo kuu la shairi hili

_____

_____

b) Sifa kubwa ya mtu kuwa mtu ni ipi?

_____

_____

c) Orodhesha tamathali za usemi zilizotumiwa katika utungo huu

i. _____

Mfano _____

Scanned by CamScanner

ii. _____

Mfano_____

d) Nini maana ya kituo bahari?

_____

_____

_____

_____

SEHEMU E (ALAMA 15)
UANDISHA/UTUNGAJI

10. Kwa maneno yasiyopungua 150 na yasiyozidi 200 andika insha kuhusu "Ajali za Barabarani"

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

Scanned by CamScanner